

UTUSHIBISHE KWA HURUMA YAKO

28e Dim. T.O.B

Musique: Charles NYENZE

Texte: Zabri 89

$\text{♩} = 40$

U - tu - shi - bi - she kwahu - ru-ma ya-ko i - li tu-sha-ngi - li - e.

5

1. Utufundishe kuzihesabu siku zetu,
tujipatie moyo wenye hekima.
Urudi, ee Bwana. Mpaka lini ?
Uwahurumie watumishi wako.

2.Utushibishe upesi kwa huruma yako,
nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote.
Utufurahishe kadiri ya siku ulizotutesa,
kadiri ya miaka tulipoona mabaya.

3.Matendo yako yaonekane kwa watumishi wako,
na utukufu wako kwa watoto wao.
Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu;
na kazi ya mikono yetu utusitawishie.